**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam**
**27 Juni 2009**

**Waliohudhuria**
Juma Ali Salehe Jongo
Elaine Baker
Omary Shabani
Juma Hassan Chibaya
Beda John Mkusu
Ally Athuman Jumbe
Shamte J Kisoma
Mohammed Samwely
Alen J Nyanginywa
George Kabogo
Bashiri Rashidi
Ally Salum
Athmani Mussa
Saidi Brashi
Filbert Mbecha
Paulo Atibu Hatibu
Hamadi Hatibu Bwaja
Husein Hamza Hamisi
Rahma Ali
Shaban Mohammed Mwalimu
Mussa Omari
Edgar R Paulo
Hamza Mohamed
Abdul H Mwaibambe

**Mgeni**
Tom Bishop

**Mazungumzo na mgeni**
Tom Bishop alijitambulisha. Ni mhandisi kutoka Uingereza na amekuja hapa Tanzania kuanzisha tawi la NGO inayoitwa Amend. Alikutana na Mejah huku Ubelgiji. Shirika hili lina lengo kuongeza usalama barabarani kwa watoto. Tayari Amend in tawi huko Ghana. Atakaa hapa mpaka mwezi wa kumi na mbili kusaidia kuanzisha tawi. Sasa anatafuta ofisi na wafanyakazi kama meneja wa mradi. UWABA tulieleza kuhusu malengo yetu na mafanyiko. Tulieleza kuhusu mradi wa kufundisha wanafunzi wa shule kuhusu usalama wa baisikeli. Tulisema tutapenda kushirikiana naye.

**Mkutano wa Tanga**
Dominata aliandika repoti kuhusu mkutano wa Tanga alimpa Filbert. Tulisema kwamba tutasikia repoti yeye atakaporudi kutoka safari nyingine ili atoe maelezo mwenyewe. Elaine alisema ni nzuri sana amevyofanya kuandika repoti hivi.

**Mradi wa Wamba**

Filbert aliandika repoti kuhusu mafunzo ya Magomeni na alisoma kwenye mkutano. Elaine ataichapa. Filbert pia alileta maswali ya evaluation.

Tulipiga mahesabu ya mafunzo na Elaine atachapa. Filbert na Hamadi walibaki na Tsh 30,000 kutoka hela ya helmet na printing ya jaketi.

Elaine atawasiliana na Imelda kuhusu mafunzo ya Temeke. George atawasiliana na shule ya Mabibo. Tutajaribu kupata contacts ya shule ya Mbondole, ambayo ni jirani na shule ya Msongola.

**Mkutano wa mashirika ya wapanda baisikeli, Nairobi**
Edgar alinunua tiketi kwa watu watatu kwenda Nairobi na Mohammed Transport kwa Tsh 150,000 kwa kutumia hela ya UWABA. Hela itarudishwa UWABA wakirudi wakishapata hela Nairobi.

Elaine aliandaa vipeperushi vya kusambaza huko.

Elaine atawasilana nao kupata jina la hoteli na namba za simu za kupiga wakati wa kufika.

**Mkutano wa usalama barabarani, Dar es Salaam**
Wanachama wengi zaidi walijiandikisha kuhudhuria. Wanachama walikubali Elaine achague nani aende kwa kuangalia idadi ya mikutano kila mwanachama aliyehudhuria, na pia tuwe na nafasi za wanawake.

Lugha itakuwa kiingereza na kifaransa lakini siyo Kiswahili. Mavazi lazima tuwe smart sana kwenye cocktail ya tarehe 7 na chakula cha jioni cha tarehe 8 kwa sababu wakubwa watakuwepo. Siku zingine tunaweza kuvaa t-shirt ya UWABA pamoja na suruali au skati ndefu.

Elaine atawauliza kuhusu saa za kuanza na kumaliza na pia kama kuna sehemu ya kuoga ili tupange usafiri. Atatoa nakala za barua ya kualika. Atapata taarifa kama tutakuwa na nafasi ya kutoa mada tarehe 9 au 10.

**Re-cycle**
Bado tunasubiri taarifa ya msamaha wa kodi kabla ya kuendelea.

**JICA**
Elaine aliwatumia JICA dondoo za mkutano, na wao walisahihisha, halafu aliweka kwenye website.

**Kongamano**
Elaine aliwasiliana na Uli Malsuis kuomba ushauri. Alisema ataongea na Christopher Japhet. Elaine aliona kwenye bao la tangazo serekali la jiji kwamba kuna mkutano kati ya madiwani na wananchi kila mwezi – tulikosa mwezi huu. Ataandika barua kuomba taarifa kwamba mkutano mwingine utakuwa lini.

**Ushirika wa Fasta Cycle courier**
Bwana Bukuku alisema tukutane naye mwezi wa saba.

**Mkutano na waziri ya miundombinu**
Tunasubiri repoti ya Mejah kuhusu mkutano wa Ubeljiji.

**Ruzuku ya Foundation for Civil Society**
Elaine aliwasiliana na FCS na walisema wameshapata maombi yetu na tutapata jibu ndani ya miezi miwili.

**Msafara**
Elaine aliandika proposal.  Edgar atawasiliana na UNEP.  Elaine atatayarisha barua kuomba udhamini kutoka wadhamini mbali mbali.

**Wimbo**
Tunasubiri CD cover.

**Video**
Bado traffic police (Mejah), na Star TV na DART (Sosthenes).  Elaine atampa contact wake TBC.

**Mambo ya hela na guta**
Elaine na Juma walienda benki walichukua Tsh 260,600.  Tsh 110,600 ilirudishwa kwa Elaine kwa hela ya chakula cha mafunzo Tsh 40,000, hela ya photocopy ya mwongozo Tsh 62,600 na hela ya picha Tsh 8,000.  Tsh 150,000 tulimpa Edgar kununua tiketi za basi ya Nairobi.

Filbert alikuwa na Tsh 3,000 pamoja na Tsh 30,000 chenji kutoka mafunzo ya Magomeni.  Dereva wa guta alileta Tsh 20,000, bado anadaiwa Tsh 8,000.  Tulilipa posho ya Juma kwa mwezi wa tano Tsh 20,000.  Elaine alitumia Tsh 4,000 kuphotocopy vipeperushi vya Nairobi na Filbert alirudisha hela yake.  Basi Filbert ana hela ya UWABA Tsh 29,000.

**Kamati**
Hamadi alisema kwamba Juma alipata discount ya Tsh 30,000 wakati wa kununua jaketi za reflecta lakini alipata resiti inayoonyesha hakuna discount na alichukua Tsh 30,000 kama hela yake binafsi.  Juma alisema ni kweli.  Elaine alisema kwamba siyo sahihi.  Hamadi alisema kwamba siyo mara ya kwanza Juma hajatumia vizuri hela.  Elaine alipendekeza tuchague upya kamati kwa sababu hatujafanya uchaguzi wa chama muda mrefu na siyo nzuri mtu afanye kazi ya kamati wakati wanachama hamwamini.  Wanachama tulikubali kwamba tufanye uchaguzi wa kamati nzima.  Tarehe ya uchaguzi utapangwa baadaye.